

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Kumb. Na. JA.9/259/01/A/507

05-04-2024

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa niaba ya **MDAs & LGAs** anapenda kuwataarifu Waombaji Kazi wote walioomba kazi kuwa usaili unatarajiwa kuendeshwa kuanzia tarehe **06-04-2024 hadi 09-04-2024** a hatimaye kuwapangia vituo vya kazi waombaji kazi watakaofaulu usaili huo. Wasailiwa wanaoitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

1. Usaili utafanyika kuanzia tarehe kama ilivyooneshwa kwenye tangazo hili muda na sehemu ambapo usaili utafanyika umeainishwa kwa kila Kada.
2. Kila msailiwa anatakiwa kufika kwenye eneo la usaili akiwa amevaa Barakoa (Mask)
3. Kila Msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi;
4. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na:- Kitambulisho cha Mkazi, Kitambulisho cha Mpiga kura, Kitambulisho cha kazi, Kitambulisho cha Uraia, Hati ya kusafiria au barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa/Kijiji unachotoka.
5. Wasailiwa wanatakiwa kufika na **VYETI VYAO HALISI, kuanzia cheti cha kuzaliwa, kidato cha IV, VI, Astashahada, Stashahada, Stashahada ya Juu, Shahada na kuendelea kutegemeana na sifa za Mwombaji.**
6. Wasailiwa watakaowasilisha **Testimonials, Provisional Results, Statement of results, hatiza matokeo za kidato cha IV na VI (form V and form VI results slips) HAVITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI.**
7. Kila msailiwa atajigharamia kwa Chakula, Usafiri na Malazi.
8. Kila Msailiwa azingatie tarehe, muda na mahali alipopangiwa kufanyia usaili.
9. Kwa waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (kama TCU, NACTE au NECTA)
10. Waombaji kazi ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo. Hivyo, wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa na kuzingatia mahitaji ya tangazo husika.
11. **Kwa kada ambazo wanatakiwa kusajiliwa na Bodi zao za Kitaaluma wanapaswa kuja na vyeti vyao Halisi vya Usajili pamoja na Leseni za kufanyia kazi.**

12. Wasailiwa wote walioitwa kwenye usaili wahakikishe wanaingia kwenye akaunti zao na kunakili namba ya mtihani kwa kuwa namba hizo hazitatolewa iku ya usaili
13. Wasailiwa wote mnajulishwa kuwa hali ya hewa ya Jiji la Dodoma ni baridi hivyo mnashauriwa kuvaa nguo zinazohimili hali ya hewa ya ubaridi.

RATIBA YA USAILI WA MCHUJO

| MWAJIRI | KADA | TAREHE YA USAILI | MAHALI |
|----------------|---|-------------------------|--|
| MDAs & LGAs | AFISA TEHAMA II (FANI YA USALAMA WA MIFUMO YA TEHAMA) | 06-04-2024 07:00 AM | USAILI HUJU UTAFANYIKA KWA NJIA YA MTANDAO (ONLINE). UTAJULISHWA VITUO VYA USAILI KUPITIA TOVUTI YA SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA. |

RATIBA YA USAILI WA VITENDO

| MWAJIRI | KADA | TAREHE YA USAILI | MAHALI |
|----------------|---|-------------------------|-------------------------|
| MDAs & LGAs | AFISA TEHAMA II (FANI YA USALAMA WA MIFUMO YA TEHAMA) | 08-04-2024 07:00 AM | DAR ES SALAAM NA DODOMA |

RATIBA YA USAILI WA MAHOJIANO

| MWAJIRI | KADA | TAREHE YA USAILI | MAHALI |
|----------------|---|-------------------------|---|
| MDAs & LGAs | AFISA TEHAMA II (FANI YA USALAMA WA MIFUMO YA TEHAMA) | 09-04-2024 07:00 AM | OFISI ZA SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA1. ENEO LA DKT. ASHA ROSE MIGIRO - DODOMA2. KIVUKONI, UTUMISHI HOUSE, (8 KIVUKONI ROAD). -DAR ES SALAAM |

MWAJIRI: MDAS & LGAS

KADA: AFISA TEHAMA II (FANI YA USALAMA WA MIFUMO YA TEHAMA)

TAREHE YA USAILI WA MCHUJO: 06-04-2024 07:00 AM

MAHALI: USAILI HUU UTAFANYIKA KWA NJIA YA MTANDAO (ONLINE), UTAJULISHWA VITUO VYA USAILI KUPITIA TOVUTI YA SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA.

TAREHE YA USAILI WA VITENDO: 08-04-2024 07:00 AM

MAHALI: DAR ES SALAAM NA DODOMA

TAREHE YA USAILI WA MAHOJIANO: 09-04-2024 07:00 AM

MAHALI: OFISI ZA SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA1. ENEO LA DKT. ASHA ROSE MIGIRO - DODOMA2. KIVUKONI, UTUMISHI HOUSE, (8 KIVUKONI ROAD). -DAR ES SALAAM

| # | JINA LA MWOMBAJI | ANUANI | # | JINA LA MWOMBAJI | ANUANI |
|---|----------------------|-------------------------------------|---|-------------------------|----------------------------|
| 1 | BERNARD ABDU MUHAMBO | P.O Box 9833, Ilala, Dar es Salaam. | 2 | RAMADHANI MOHAMED GAZI. | P.O Box 178, Tanga, Tanga. |

LIMETOLEWA NA;

KATIBU

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA